

# Pambazuko *Ukweli Hauna Kutu*

Toleo Namba 009

Jumatatu Septemba 05-11, 2022

**Washauri wa jikoni wa Samia wako wapi?-Uk.4**



**Hawa leo kuamua hatma Kenya Uk. 7**



**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

### Amani itamalaki Kenya

**L**EO - Jumatatu ya Septemba 5, 2022, itaingia katika kumbukumbu za Kenya kuwa ni miongoni mwa siku muhimu katika historia za nchi hiyo baada ya majaji saba wa mahakama ya upeo watakapoamua hatma ya uongozi wa nchi hiyo.

Kwa siku kadhaa, majaji hao wamekuwa wakisikiliza hoja za mawakili wa Raila Odinga, mgombea urais ambaye anapinga kutangazwa kwa William Ruto kuwa mshindi wa nafasi ya urais uliofanyika Agosti 9, mwaka huu baada ya matokeo ya uchaguzi mkuu kutangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC).

Odinga alikwenda katika mahakama hiyo kutimiza haki yake ya kikatiba ili kupigania kile anachoamini; kwamba mchakato wa kupokea, kuhesabu na hata kutangazwa kwa mshindi wa urais, haukuwa wa haki na ulishindwa kuwapa Wakenya mshindi halali.

Madai ya Odinga kupitia kwa mawakili wake ni kwamba kulikuwapo wizi wa kura, kuchezeza kwa mfumo wa kielektroniki katika kukusanya kura halali na hata kutangazwa kwa mshindi.

Hivyo, Odinga na timu yake ya wanasheria wanadai kutangazwa kwamba yeye ndiye mshindi halali ama kurudiwa kwa zoezi la kupiga kura ili hatimaye apatikane mshindi ambaye ni chaguo la Wakenya.

Baada ya kuwasilisha hoja zao, mawakili wa Ruto nao waliwasilisha hoja kinzani zao kupinga kile kilichoombwa na Odinga na kueleza kwamba hakukuwepo dosari zozote katika mchakato wa kumpata

rais wa nchi hiyo. Pamoja na Ruto, pia mawakili wa IEBC nao walitoa pingamizi na hoja zao, wakieleza namna ilivyokuwa vigumu kuchezea mfumo na kuwa aliyetangazwa ndiyo mshindi halali; Ruto.

Kazi za mawakili na maswali ya majaji ilimalizika Ijumaa iliyopita na kazi ikabaki moja kubwa, majaji kuketi na kuanza kuchambua hoja zote, kupima na kuangalia uhalali wa ushahidi ili kutoa hukumu ya haki.

Matokeo ya kazi ya majaji hao saba inahitimishwa leo ambapo kutakuwa na hukumu yenye kutarajiwa kuwa na moja kati ya uamuzi huu; kuamua kurudia uchaguzi ama kuelekeza tume kumtangaza mshindi halali kwa vigezo walivyoona vinastahili.


Tunawaomba wananchi wa Kenya, kuendelea kuwa na subra, kukumbatia amani na kupokea kwa utulivu mkubwa matokeo yoyote ya majaji hao wa korti kuu.

Ukomavu wa Kenya katika kulinda amani ya nchi yao utaonekana leo wakati wakisubiri kutangazwa kwa hukumu inayotarajiwa kuwa ya haki kwa wagombea na wafuasi wao - lakini kwa Wakenya wote, bila kujali waliopiga kura ama wengine.

Kila anayependa amani na utuliviu, lazima ataungana na sisi kuombea na kusisitiza amani kwa wananchi wote wa Kenya wakati hukumu hiyo ikitangazwa.

Sisi katika Pambazuko, tuna imani kubwa na Wakenya wakati wanasubiri kwa hamu na gamu kuyapata matokeo ya kazi kubwa waliyoifanya ya kampeni, kupigakura na sasa kusubiri kupata hukumu ya korti kuu.

Kila jema kwa Wakenya na kwa wana wa Afrika Mashariki wote.



## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: [pambazuko1@protonmail.com](mailto:pambazuko1@protonmail.com) ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



*“Umoja hautatufanya kuwa tajiri, lakini unaweza kuiepusha Afrika na watu wa Afrika kutoheshimiwa na kudhalilishwa na mataifa mengine, hasa tajiri” - kutoka katika hotuba ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoitoa Accra, Ghana, Machi 6, 1997.*

●Wiki iliyopita, ilisahaulika kuweka mzungumzaji, tunaomba radhi kwa kosa hili- Mhariri.

---

### Washauri wa jikoni wa Samia wako wapi?

Na Simon MKINA

**M**AANDIKO na hadithi kadhaa ndani ya Vitabu Vitakatifu; Biblia na Quran, yanaeleza kwamba sauti ya wengi, iwe inatoka nyikani, upenuni na hata kwenye viambaza, ni sauti ya Mungu.

Hayo pia yanapazwa na wahenga ambao maneno yao tumeyasoma ama kusimuliwa - kwamba nao wanaamini sauti, na pengine vilio vya wengi ni msukumo wa nguvu moja kuelezea furaha au huzuni.

Wanapocheka wengi, basi mbingu hufurahi pamoja nao na wanapolia, mbingu hiyohiyo, hulia pamoja nao.

Hivi sasa Watanzania wanalia. Wanamwaga chozi la uchungu wakidhani kwamba serikali yao imeshindwa kuwasikiliza na kuwafuta chozi.

Wanalizwa na mlolongo wa kodi na rundo la tozo kila wanapopata huduma ama kununua bidhaa. Wingi huu wa makato ya fedha zao, unachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza kile walichokuwa wakipata awali.

Hulka ya Watanzania siyo kulalama. Watanzania siyo wabishi na Watanzania kamwe siyo watu wa kubweteka na kulialia, lakini hili la tozo-umiza na wingi wa kodi, zingine wakilazimika kulipa mara mbilimbili, hakika limewagusa mtima.

Siyo kwamba Watanzania wanagomea kodi au tozo, la hash! Wanatambua umuhimu wa kulipa kodi ili kuiwezesha serikali kupata mapato ya kuendesha nchi, lakini wanapokamuliwa kiasi kikubwa cha kuwaumiza, wanapaza sauti, wanaandamana kimoyomoyo na kulaani.

Wengi wanajuiliza, kwanini kuwepo kodi lukuki na tozo-umiza nyingi ambazo serikali inazipigia chapuo kuonyesha kwamba ni muhimu zaidi hata kama zinawaumiza?

Wanaliza, kama lengo ni kukusanya kingi kwa maendeleo makubwa, kwanini



Rais Samia Suluhu Hassan

basi, matumizi makubwa na yasiyokuwa ya lazima kwa watendaji serikalini yasiyopunguzwe?

Kuna haja gani ya kuwa na bajeti kubwa ya magari ya kifahari kwa watendaji wa serikali? Kuna haja gani ya kuendelea kulipa fedha nyingi kwa wanasiasa – hasa wabunge? Kuna haja gani ya kuendelea kuagiza ndege za serikali wakati biashara ya anga inaporomoka na imeshindwa kusimamiwa vyema hapa kwetu?

Wanahoji, Rais Samia Suluhu Hassan yuko wapi kuwafuta chozi? Wanaingwa na matumaini kuwa huenda kimya chake kina mshindo mkuu, ataibuka na kuja na kauli fupi tu; “ondoa tozo-umiza.” Ili familia zao zipone. Lakini itakuwa lini? Wakati wanaendelea kulia? Hofu inatanda tena!

Wanahoji, hivi nani wa kumtonya Rais Samia kuwa huenda kuna mazonge yanaundwa yakiwa na lengo la kuvuruga mahali?

Wanatizika wakiuliza – “hivi washauri wa jikoni wa Rais Samia wako wapi na wanashauri nini katika hili la kufuta chozi.”

Wanaomba kama wapo awasikilize na ikimpendeza achukue hatua haraka ili Tanzania isonge, na kuacha ama kupunguza kuwa taifa la walalamikaji na watu wenye mijadala ya aina moja tu; kulalama kuhusu maumivu ya tozo.

---

## Kizungumkuti tozo kwenye Luku

Na Betty MASSANJA

**N**ISHATI ya umeme ni muhimu kwa binadamu. Umuhimu wake uko katika kurahisisha maisha, hivyo inapaswa kuwa bidhaa inayoweza kuwa nafuu ya bei, pamoja na upatikanaji wake.

Hata hivyo, bei ya nishati hiyo nchini Tanzania kwa sasa inakatisha tamaa ya maisha bora, hasa kwa raia wa vipato vya chini kutokana na mlolongo wa kodi zinazotowza kupitia malipo ya Luku.

Imebainika kuwa mfumo wa Luku unatumika kufanya makato kadhaa yanayochukua karibu asilimia 50 ya fedha ya kila mteja, kwa ajili ya serikali. Makato hayo ni kama ifuatavyo, asilimia zikiwa kwenye mabano; kodi ya VAT (18%), kodi ya EWURA (1%), kodi ya REA (3%), na kulipa deni (50%).

Ipo miamala dhahiri miwili kwa ajili ya kubfika hitimisho kwamba tozo ni kubwa na zinaumiza; moja ni wa mteja aliyenunua umeme wa Sh. 7, 000 - Agosti 27, mwaka huu, alipata mchanganuo wa makato ufuatao: Umeme wa matumizi (41%) Sh. 2,868.86; kodi ya VAT (18%) Sh. 516.39; kodi ya EWURA (1%) Sh. 28.69; kodi ya REA (3%) Sh. 86.06; kulipa deni (50%) Sh. 3,500.00. Deni hili ni sawa na asilimia 50 ya fedha zake zote.

Mteja mwingine aliyenunua umeme wa Sh. 6,000 siku hiyohiyo, ambaye

alipata mchanganuo wa makato ufuatao; umeme wa matumizi (41%) Sh. 2,459.02; kodi ya VAT (18%) Sh. 442.62; kodi ya EWURA (1%) Sh. 24.59; kodi ya REA (3%) Sh. 73.77; na kulipa deni (50%) Sh. 3,000.

Swali linaloulizwa na wananchi hapa ni hili: Je, uhalali wa serikali kuchukua asilimia 50 ya fedha kwa wateja wa umeme kupitia mfumo wa Luku unatoka wapi?

Hata hivyo, Pambazuko limeelezwa na ofisa mmoja wa Tanesco kwamba deni linaloonekana katika makato, ni madeni ya nyuma ambayo wenye mita walikuwa wakidaiwa kabla ya kuanza kwa matumizi ya mfumo wa Luku.

Pamoja na majibu haya, bado wahusika wanahoji, kwanini ikatwe asilimia 50 kwa mkupuo, kwani kufanya hivyo ni kumuumiza zaidi mteja ambaye anaweza asiwe aliyeacha deni.

Malalamiko hayo yanakuja katika kipindi ambacho Watanzania wengi wanalia kutokana na mlundikano wa tozo za miamala ndani ya sekta ya fedha kwa upande mmoja na mawasiliano ya simu ya mikononi, kwa upande mwingine.

Ni wakati muafaka sasa kwa serikali kuja na utaratibu mzuri wa kupunguza ukali wa maisha kwa kupunguza kodi nyingi na tozo – umiza zinazolalamikiwa na wananchi.



Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba

### Umbo la mwalimu lavuruga wazazi



**W**AZAZI katika shule moja ya wanafunzi wa awali Jimbo la New Jersey, Marekani wameulalamikia uongozi wa shule hiyo kutokana na kuwa na mwalimu mwenye umbo “zuri zaidi.”

Barua iliyoandikwa kwa uongozi wa shule hiyo na kuonwa na gazeti la New York Post, inaeleza wasiwasi wa wazazi hao kuhusu maadili na uwezo wa watoto wao kusoma kutokana na umbo hilo.

Wazazi hao wanadai kwamba mwalimu huyo, ambaye jina lake limefichwa na gazeti hilo, amekuwa akivaa “mavazi yasiyofaa” yanayoonyesha umbo lake lenye “kuvutia,” hivyo wanataka afukuzwe au aamue kuvaa mavazi yenye staha.

Sheria za jimbo hili zinakataza mfanyakazi yeyote kufukuzwa ama kunywanyaswa kutokana na umbo lake na kwamba hata “kumsema” mtu mwenye umbo kubwa au dogo, ama vinginevyo ni kosa kisheria.

Baadaye mwalimu huyo alitumia mtandao wake wa Instagram kuwajibu wazazi hao kwamba yeye hana uamuzi kwenye umbo lake na kuwa hakuchagua kuzaliwa hivyo, bali ni mapenzi ya Mungu.

Hata hivyo, amekubali kuvaa mavazi

yenye kulegea ili kuzuia umbo lake – lenye kuitwa “la nyigu,” ili kutowakwaza wazazi na hata walimu wenzake.

*New Jersey (New York Post)*

### Ubaguzi Afrika Kusini tishio

**S**ASA ni dhahiri kuwa wananchi wa nchi za Afrika waliokimbilia nchini Afrika Kusini kwa lengo la kutafuta maisha bora, uhai wao uko hatarini.

Idadi kubwa ya vijana wamekuwa wakivamia na kupora mali katika biashara za wageni, kutishia kuchoma moto makazi yao na zaidi kuwapiga kila wanapokutana nao mitaani.

Hali ni mbaya katika miji mikubwa nchini humo ikiwamo Johannesburg na Durban. Hata hivyo, hali ni tofauti kwenye miji inayokaliwa na wazungu wengi.

Watu kutoka Zimbabwe ndiyo waathirika wakubwa wa sekeseke hili na wanaeleza kuishi maisha ya hofu kutokana na kubaguliwa huko.

Sababu zinazolezwa na vijana wa Afrika Kusini kufukuza wageni hao ni ajira. Kwamba wageni wamekuwa wakikubali kufanya kazi kwa ujira mdogo na mazingira yasiyoridhisha, wakati wao wanakataa.

*Limpopo (DM)*

### Wasichana wateswa Uarabuni

**W**ASICHANA kutoka nchi za Kenya na Uganda wanaoenda nchi za Falme za Kiarabu, wamekuwa wakigeuzwa watumwa, imegundulika.

Habari kutoka Dubai zinaeleza kuwa wasichana hao wanaorubuniwa maisha mazuri na kampuni zinazowapeleka huko, wamekuwa wakiteswa na wengine kuuawa na waajiri wao, huku miili yao ikifichwa au kutelekezwa hosipitali.

*Dubai (mtandao)*



## Watu saba leo kuamua nani rais

Na Mwandishi WETU

**L**EO Wakenya watajua hatma ya Luongozi wa nchi yao, baada ya uamuzi wa majaji saba wa Mahakama ya Juu (Upeo) kuamua nani anakuwa rais.

Uamuzi huo ama utampa ofisi kuu, RAIS Mteule William Ruto au kumpa mkongoyo Raila Odinga kwenda kupumzika baada ya kupigania kiti hicho kwa zaidi ya miaka 30.

Hata hivyo, mahakama hiyo inaweza pia kutangaza kurejewa kwa uchaguzi huo uliofanyika Agosti 9, 2022 na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) kumtangaza Ruto kuwa mshindi.

Odinga alikwenda mahakamani kupinga matokeo hayo, huku akieleza kuwepo kwa sababu lukuki, ikiwamo wizi wa kura zake, kuhujumiwa kwa mfumo wa kielektroniki kukusanya matokeo na mengineyo.

Tangu juzi, majaji saba wa mahakama hiyo wako mahali kusikojulikana wakimendelea kupitia hoja, marejeo na hatimaye leo kutangaza uamuzi wao.

Ikiwa uamuzi wao utaelekeza kutangazwa kwa rais, watatoa amri kwa tume kufanya kazi hiyo. Rais huyo ataapishwa Septemba 13, mwaka huu.

Jaji Mkuu Martha Koome na majaji;



William Ruto



Raila Odinga

Philomena Mbete Mwilu, Mohamed Ibrahim, Dkt. Smokin Wanjala, Njoki Susanna Ndung'u, Isaac Lenaola na William Ouko ndiyo wenye kutoa hukumu hiyo.

Katika matokeo yaliyotangazwa na mwenyekiti wa IEBC, Ruto alishinda kwa kuzoa kura 7, 176, 142 (asilimia 50.49 ya kura), huku Odinga akitangazwa kupata kura 6, 942, 930 (asilimia 48.85).

Mawakili wa pande zote walihitimisha kuwasilisha hoja zao za mwisho katika jitihada za kushawishi majaji kukubaliana na kile walichoamini kwenye shauri hilo.

Tayari Jaji Mkuu Koome ametoa hakikisho kuwa yeye na wenzake watatoa uamuzi wa haki utakaozingatia Katiba na sheria.

Katika hotuba ya mwisho, Jaji aliwaomba mawakili wa pande zote na Wakenya kwa ujumla kuwaombea ili watoe uamuzi wenye “busara kubwa na unaoendeleza demokrasia.”

“Kazi ambayo, tumemaliza ndio ilikuwa ngumu zaidi kuliko ile kazi ambayo tunaelekea kufanya ya kuandaa uamuzi mkubwa utakaokuza misingi ya demokrasia,” alisema Koome.

Kauli yake iliungwa mkono na Naibu wake, Jaji Mwilu.

---

# Utengenezaji wa siasa

Na Askofu Stephen MUNGA

**N**ADHARIA juu ya uundwaji wa jamii za kisiasa zinatofautiana huku baadhi ya waundaji mahiri wa nadharia hizo wakikubaliana juu ya lengo kuu la uundaji huo.

Lengo hilo ni uunganishwaji wa watu kuwa jamii na kutengeneza misingi thabiti ya kutunza amani. Njia mojawapo ya kufikia lengo hilo ilikuwa ni kujenga misingi ya utendaji haki sawa kwa watu wote.

Mwanzo huu wa uundwaji wa jamii waweza kufananishwa na kile John Rawls alichaita ‘nafasi ya asili’ katika kitabu chake *A Theory of Justice* (Nadharia ya Haki). Hiyo ni nafasi ambayo kuna usawa kabisa kwa watu wote na kutoka hapo waanze kuunda jamii yenye haki kwa kutengeneza misingi yake kwa ushirika pasipo pepote kuwa juu ya mwingine.

Msemo kama ule usemao kuwa mtu ni mnyama wa siasa (man is a political animal); na mtu ni mnyama wa jamii (man is a social animal), kama nilivyosema huko nyuma; ili mtu athibitishwe utu wake, anahitajika mtu mwingine zaidi kufanya hivyo.

Muhimu pia ni kwamba ili kupata ulinzi na kuhakikisha usalama wa kuishi kwake mtu alihitaji kuungana na wengine kutengeneza jamii.

Pamoja na kutengeneza jamii ilihitajika miongozo ya jinsi ya kuishi pamoja bila kuumizana au kuangamizana. Nidokeze kuwa uwepo wa jamii unakuwa haki ya kila mmoja kuwemo humo na ni wajibu wa kila mmoja kuifanya iwepo na iwe na ubora.

Kwa hiyo uundwaji wa jamii ulikuwa na baraka zake lakini pia ulikuwa na changamoto zake. Bila shaka changamoto ya kwanza ni juu ya mchanganyiko wa watu wale wanaounganishwa kuwa jamii moja. Katika nadharia zile za awali picha inayoonekana ni kama vile walikuwepo watu lakini kila mmoja aliishi kivyake bila uhusiano na wengine.



*Mwanasiasa*

Katika nyakati za baadae ambapo jamii tayari zimekuwepo nadharia huzingatia uhifadhi wa ubora wa jamii ili itimize lengo lake kuu la kutunza amani kwa kusimamia haki na usalama. Katika mitazamo yote miwili changamoto kubwa ni namna ya kuwa na vigenzo vya kuchuja ubora wa watu wenyewe ili watengeneze jamii bora. Sheria na taratibu zilitengenezwa ili kuwa miongozo ya kulinda tunu hizo.

Kwa hiyo basi, katika utengenezaji wa siasa safi ‘nafasi ya asili’ ni mahali tunapotakiwa kurejea tena na tena ili kwenda pamoja kwa kuelewana na pasipo kukandamizana. Nadharia hii ukiitazama vizuri uatona kwamba imebeba msingi mkubwa wa fikra za kidemokrasia na kutupilia nje zile za kiimla. Kinachotakikana hapo ni aina ya watu mfano wa yule tuliyemtengeneza katika gurudumu lile la “watu” katika makala zilizopita.

---





Na Evarist Chahali  
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

## Kongole Rais Samia kwa mageuzi haya

**K**UNA msemu kwamba “historia khandikwa wakati macho yameelekezwa kwingineko.” Na hicho ndicho – kwa mtazamo wangu – kilichojiri wiki iliyopita katika hafla ya kuwaapisha majaji na Kamishna Jenerali wa Magezea jijini Dodoma.

Katika hotuba yake baada ya uapisho huo, Rais Samia Suluhu Hassan aliongelea suala ambalo yayumkinika kulitaja kuwa ni “geni” katika nchi nyingi duniani, ikiwa ni pamoja na zile zilizoendelea. Suala hilo ni haki za wafungwa.

Ni ukweli usiofichika kwamba katika nchi nyingi, kifungo hulenga kumuadhibu mfungwa pasipo kujali haki za mfungwa husika wala kujihangaisha kuwa mustakabali wa mfungwa huyo pindi akimaliza kifungo.

Matokeo yake, wafungwa wengi hujikuta wakirudi tena jela kwa sababu muda waliotumikia kifungo ulihusisha zaidi kuwaadhibu kuliko kuwarekebisha.

Kubwa zaidi katika hotuba ya Rais Samia lilikuwa mkazo aliouweka, siyo tu kwenye umuhimu wa haki za wafungwa kuthaminiwa, bali suala zima la haki-jinai.

Huu ni mtazamo bora kabisa kwa sababu ni sawa na “kuua ndege wawili kwa jiwe moja.” Kwa upande mmoja, kuzingatia haki-jinai kutawezesha haki za binadamu za wafungwa kuheshimiwa, na kwa upande mwingine, wafungwa wataandaliwa mazingira ya kuwawezesha kuwa na mchango chanya kwa jamii baada ya kumaliza vifungo vyao.

Kwa huku nchi za Magharibi, suala la haki-jinai limekuwa miongoni mwa vipaumbele vikubwa katika siku za hivi karibuni. Nchini Marekani, mhalaki Kim Kardashian, amekuwa mmoja wa wanaharakati wa haki jinai, hususan



Rais Samia Suluhu Hassan

kwenye kusisitiza mabadiliko ya mfumo wa magezea unaowakandamiza zaidi Wamarekani Weusi.

Licha ya kuguswa na tamko hilo la Rais Samia, kwa mara nyingine, nilipatwa na hisia kuwa “mazuri yake hayapewi uzito stahiki” kulinganisha na “mapungufu” ya utawala wake.

Kama ilivyokuwa baada ya kutangaza kuunda sekretarieti na tume ya kufuatilia utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama, tukio la kihistoria kwa Tanzania yetu, jitihada zake kuhusu haki jinai pia “hazikupokewa kwa uzito stahili” licha ya ukweli kwamba kiongozi huyo alikuwa akindika historia mpya.

Nadhani tatizo lipo kwa baadhi ya watendaji ambapo wengi wanajibidiisha zaidi “kumsifia kwa maneno matupu” badala ya kuongelea rekodi kama hizo mbili nilizozitaja – security sector reform (mageuzi kwenye sekta ya usalama) na criminal justice reform (mageuzi kwenye haki jinai).

**Hongera Rais Samia kwa rekodi  
hisi muhimu**

---

### Nyama kutengenezwa viwandani

**Na Mwandishi WETU**

**M**AENDELEO ya sayansi na teknolojia yanakimbia kwa kasi. Kila kukicha kuna mabadiliko makubwa, siyo katika mashine na mitambo tu, bali hata kwenye vyakula na vinywaji.

Zamani ilikuwa ndoto kufikiri kuwepo uwezekano wa kupatikana sukari isiyotokana na miwa, matunda na maua, lakini leo ipo. Kuna sukari ya mahindi na hata viazi. Wamarekani wengi sasa wanatumia zaidi sukari kutoka kwenye nafaka.

Kama hiyo haitoshi, wanasayansi wa Israel sasa wanakuja na nyama ambayo haitokani na wanyama wa kufugwa wala wa porini. Ni nyama inayotengenezwa viwandani.

Nyama hiyo, inaelezwa kuwa na ladha, rangi, mafuta, seli, misuli na alama zote za nyama ya ng'ombe ambayo imezoeleka tangu enzi na enzi.

Tayari Israel ina viwanda vikubwa vitatu ambavyo vinatangeneza nyama ya ng'ombe bila kuchinja wanyama hao waliozoeleka kufugwa na binadamu. Viwanda hivyo ni MeaTech3D, Future Meat Technologies na Aleph Farms. Kiwanda kingine kiko Uholanzi, kikitwa Mosa Meat.

Nyama inayotengenezwa na viwanda hivyo huanza kuandaliwa kwa kuchukua seli za misuli na mafuta halisi, inayotokana na sampuli za tishu zilizochukuliwa kutoka kwa ng'ombe halisi. Wakati wa kuchukua sampuli hizo, ng'ombe hachinjwi wala "hateswi," bali sindano nyembamba hutumika.

Inaelezwa kwamba baada ya kuchukuliwa kwa seli za shina za ng'ombe hai, huchanganywa kisayansi na tishu zingine zisisokuwa na madhara kwa mwili wa binadamu kwa ajili ya kuanza kutunisha nyama ya kiwandani.

Pamoja na kwamba viwanda vingi vinaficha tishu zinazotumika na kueleza kwamba hazina madhara kwa binadamu, lakini inaaminika kuwa ngano

hutumika, huku aina fulani ya nyasi ikijumuishwa. Nyasi hizo hazijawekwa wazi. Pia inaelezwa kwamba nyama hiyo hujumuisha kiwango cha kutosha cha ufuta.

Kampuni nyingi za vyakula za Marekani na Ulaya, zinaelekeza mitaji yake kwenye teknolojia hiyo ya uzalishaji wa nyama bila kufuga wala kuchinja ng'ombe halisi.

#### **Wataalamu wa afya wanasemaje?**

Wataalam wa lishe wa Israel, Marekani, Uingereza, Uholanzi na taasisi za lishe za nchi hizo pamoja na Canada, zimeridhia kuuzwa na kutumika kwa nyama hiyo ambayo inaelezwa kutokuwa na shaka kwa binadamu.

Taarifa zinaeleza kuwa nyama hiyo ya viwandani, ina kiwango cha mafuta na virutubisho vingine muhimu, vinavyokubalika kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Seren Kell, ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Kusimamia Ubora wa Vyakula Ulaya (GFI) anaeleza kwamba nyama hiyo haina madhara na kuwa inatarajiwa kuendelea kuboreshwa zaidi ili kila mtu aweze kula bila kupata madhara.


"Unajua nyama ya ng'ombe wanaofugwa inaweza kuwa na madhara mengi kiafya, lakini nyama ya ng'ombe inayozalishwa sasa viwandani, ni bora zaidi. Watu wasiwe na wasiwasi na usalama wake, ni timamu kabisa," anaongeza mtaalamu huyo wa lishe.

Nyama ya kwanza kutengenezwa kiwandani iliyokuzwa kutoka kwenye seli ilitolewa Desemba 2018 na kampuni nyingine ya Israeli, Aleph Farms, ingawa kampuni hiyo ilisema wakati huo kwamba ladha ya nyama hiyo haikuwa sawa kabisa na ng'ombe halisi. Hata hivyo, imeendelea kuiboresha ili kuwa sawa na nyama halisi iliyozoeleka na sasa imeridhika na kiwango kinachotakiwa.

#### **Itatosheleza mahitaji?**

Ulaji wa nyama ya ng'ombe wa

## Nyama kutengenezwa viwandani



Mitambo ya kutengeneza nyama kiwandani (picha na FUTURE Meet)

kufugwa imekuwa ikipungua kwa kasi duniani kutokana na maelezo ya kuwepo kwa madhara ya kiafya kwa wanaokula kupita kiasi.

Taarifa kutoka Wizara ya Kilimo (ikijumuisha mifugo, misitu) ya Marekani (USDA) inaelezwa kuwa ulaji wa nyama kwa mwaka juzi, 2020, ulipungua kwa kiwango cha tani 398,000 ikilinganishwa na mwaka 2021, ambapo jumla ya tani milioni 59.1 za nyama ya ng'ombe zilitafunwa.

Tani hizo za nyama ni sawa na ng'ombe 591,000 wenye uzito wa kilo 100, ingawa wengi, hasa wanaofugwa kitaalamu hufikia hata kilo 350 hadi 500.

Kupungua kwa ulaji huo kunapunguzwa zaidi na wataalamu wengi wa afya wanaoeneza taarifa kuwa ulaji zaidi wa nyama ya ng'ombe ni hatari, kwani huongeza uzito kwa kasi.

Nchi inayoongoza kwa ulaji mkubwa wa nyama ni Marekani, ambao hutafuna nyama tani milioni 12 kwa mwaka. Ikifuatiwa na China inayotafuna nyama tani milioni 9. Takwimu za mwaka huu zinaeleza kuwa Marekani ina watu milioni 332, wakati China ina idadi ya watu wanaofikia bilioni 1.4.

Wenye viwanda vya kutengeneza nyama, wanadai kuwa mahitaji ya nyama hiyo yatatoshelezwa kwa kuwa wanajipanga kuongeza mitaji na utalaam

zaidi.

### Ulaji wa nyama Tanzania

Pamoja na Tanzania kuwa na mifugo mingi zaidi Afrika, ikiwa ya pili baada ya Ethiopia, bado wananchi wake hawali nyama ya kutosha.

Bodi ya Nyama Tanzania inasema bado ulaji wa nyama upo chini ambapo kulingana na viwango vya Shirika la Afya Duniani (FAO) mtu anatakiwa kula kilo 50 kwa mwaka, ambapo kwa Tanzania watu wanakula kilo 15 tu kwa mwaka.

Bodi hiyo ya nyama inaeleza kwa sasa Tanzania ina ng'ombe milioni 30.5, mbuzi milioni 18.8, kondoo milioni 5.3, kuku wa asili milioni 38.2 na kuku wa kisasa milioni 36.9.

### Nchi masikini kufikiwa lini?

Inaelezwa kuwa itachukua muda mrefu kidogo kwa nchi masikini, hasa kutoka Afrika – Tanzania ikiwamo kufikiwa na teknolojia hiyo, ingawa nyama ya ng'ombe ya viwandani itafika mapema zaidi kupitia maduka makubwa (supermarkets).

Sharon Fima, Mkurugenzi Mtendaji wa MeaTech3D, anasema; teknolojia ya kutengeneza nyama inahitaji mtaji mkubwa, lakini ni uwekezaji unaokua kwa kasi kutokana na kuwepo kwa mahitaji ya nyama safi na bora kwa afya ya binadamu.

### Maboresho yaguse Idara ya Usalama

Na Godwin CHILEWA

**K**ATIKA maboresho ya vyombo vya kulinzi na usalama yanayoendelea kufanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, imani ya wananchi ni kwamba Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) nayo itaguswa.

Ni wazi kuwa, kama ilivyo kwenye majeshi, taasisi na idara zingine za usalama, TISS kunahitajika maboresho makubwa ili iweze kufanya kazi zake kwa weledi na kuaminika.

Kwanza inapaswa ifanye marekebisho makubwa katika utaratibu wake wa ajira na mafunzo ili kupata maafisa bora, wenye nidhamu, na watakaozingatia kanuni na miiko ya utendaji wa idara.

Katika kutimiza hili, idara inapaswa kuondoa ubinafsi unaosababisha kuajiriwa kwa ndugu na jamaa wa maofisa wa idara, hata kama watu hao hawana sifa stahiki za kuwa maofisa. Ni muhimu kurugenzi ya uajiri na mafunzo katika idara (DRRT) ihakikishe wote wanaopata nafasi hizo wanapitishwa katika chekeche la kuwachuja bila kujali wahanusiana na nani.

Pamoja na hilo idara iboresha mafunzo ya awali ya vijana wanaojuunga na idara ili waweze kuwa na sifa stahiki za kuitwa maafisa wa idara. Miaka ya nyuma (hasa ya 1980), idara ilikuwa ikisifika kwa kuwa na mafunzo magumu, na ya uhakika kiasi cha maofisa wake kuheshimika kila kona.

Haya hivyo, kadri miaka ilivyosonga mbele mafunzo hayo yameelekea kulegezwa kiasi cha kuidhalilisha idara. Ni muhimu maafisa wafundishwe mafunzo ya kijeshi, mbinu za kujilinda kwa mikono mitupu na mengine yote yanayopaswa ofisa wa idara hiyo kujua kwa undani, siyo kubabaisha tu.

Mojawapo ya mambo yanayoweza kukwamisha utendaji wa idara ni usimamizi wa maofisa wake, hasa walioko mikoani na wilayani. Maeneo mengi ya huko kuna mambo mengi



Rais Samia Suluhu Hassan

yanayoidhalilisha idara kwa kuwa baadhi ya walioteuliwa wasiokuwa na uwezo wa kuongoza vituo hivyo.

Miaka ya nyuma jambo hili lilisababisha migomo baridi kila ilipoonekana ofisa aliyepewa wadhifa ana cheo cha chini, na elimu ndogo kuliko aliowakuta kituoni. Idara ilijaribu kurekebisha hili kwa kuweka utaratibu uliotaka ofisa anayeteuliwa kupewa wadhifa fulani awe na shahada ya chuo kikuu, na apandishwe cheo mara mbili ili kufikia ngazi inayohitajika kushika wadhifa ule.

Hata hivyo, utaratibu huu ulisababisha matatizo makubwa zaidi ya kiutendaji na malalamiko. Kwanza, vijana wengi walipandishwa vyeo kwa kasi na kupewa nafasi za juu bila kuzingatia uwezo wao kazini. Pili, vijana hao waliposhindwa majukumu hayo mazito, walibadilishiwa kazi (kupewa kazi nyepesi) bila kupunguzwa vyeo walivyopewa kwa haraka na hivyo kuendelea kulipwa mishahara mikubwa wasiyostahili.

Hali hii, wakati maboresho yakiandaliwa, ni vyema ikazingatiwa ili kuepusha idara kuwa na watu wasiokuwa na uwezo kusaidia nchi.

**Mwandishi aliwahi kuwa ofisa wa TISS kwa muda mrefu kabla ya kuhamia Marekani kwa shughuli zake za kanisa.**

## Utendaji mbovu waigharimu SMZ

Na Mwandishi Maalum, Zanzibar

**U**TENDAJI usiozingatia kanuni na taratibu- hasa za fedha ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) unaigharimu nchi kwa kushindwa kuhudumia wananchi ipasavyo.

Gazeti hili, Pambazuko limebaini kuwa utendaji huo umekuwa ukisababisha upotevu mkubwa wa fedha serikalini na kunufaisha kundi dogo la wajanja.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya serikali ikiwemo Hazina, ubadhirifu wa fedha za serikali umezaa tatizo sugu la nakisi kwenye fungu maalum linalotumika kugharamia shughuli za serikali katika wizara na ofisi maalum zilizo chini ya Ofisi ya Rais.

Fungu hilo litwalo 'matumizi mengineyo' - (OC), limekuwa na upungufu mkubwa wa fedha hali inayosababisha kuzorota kwa shughuli za kila siku serikalini.

"Hili jambo siyo busara hata kidogo kulichukulia kwa wepesi. Unapokosa fedha za kutosha kwenye fungu la OC, maana yake halisi ni serikali kushindwa kuhudumia umma," anasema ofisa mwandamizi aliyeko Hazina.

Ofisa huyo aliyeshurutisha kutotajwa jina lake anaeleza haya ndani ya simulizi za kuongezeka kwa ufisadi serikalini kufuatia ripoti ya ukaguzi ya Mdhidhibi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Taarifa za vyanzo zinataja kuwa fungu la "matumizi mengineyo" linakidhi kiasi cha asilimia 30 tu ya mahitaji halisi baada ya kutimia kwa fungu la mishahara ya watumishi wa serikali.

Inaelezwa zaidi kwamba fungu la mishahara lazima litimie hata iweje, maana kushindwa kulipa mishahara watumishi, ni kosa la jinai.

Hata hivyo, taarifa zinaeleza kuwa baada ya SMZ kulipa mishahara, Hazina hubaki na fedha kiasi kidogo kinachokusanywa na serikali kama kodi.

Huku vyanzo vikilalamikia ukubwa wa



Rais Mwinyi

serikali unaoongeza mzigo wa matumizi, taarifa zinasema kila mwezi mishahara inahitaji kiasi cha Sh. bilioni 50 kwa wafanyakazi wake wote - mawizarani na kwenye mashirika na taasisi zake zikiwemo idara maalum za SMZ.

"Pamoja na ukubwa wa serikali, lakini matumizi mabaya ya fedha za umma, imekuwa ni jambo la kawaida, na wakubwa hawatilii maanani shughuli zingine, isipokuwa zile zenye maslahi binafsi, sasa ni shida," anasema ofisa mmoja ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2020/2021 iliyotolewa Ijumaa iliyopita, ilieleza kuwepo kwa ufisadi mkubwa wa fedha za serikali na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi akataka "lazima hatua za kisheria zichukuliwe vinginevyo ni kuendelea kutowatendea haki wananchi."

Rais Mwinyi aliilaumu Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca) kuwa imeshindwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kumpeleka angalau mtuhumiwa mmoja mahakamani japokuwa baadhi yao wamekiri na kurudisha fedha.

Alitaka uongozi wa mamlaka kujitathmini- kauli iliyomsukuma Mkurugenzi Mkuu wa Zaeca, Ahmed Khamis Makarani kuandika barua ya kujiuzulu. Rais aliridhia uamuzi huo.

### Tutakumbuka Daima...



*Kwamba Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, aliwahi kusakata rhumba na mwanamke hodari na shupavu aliyesaidia kuhamasisha wanawake kuukataa ukoloni, Titi Mohammed. Mkutubi wa Pambazuko ameshindwa kupata taarifa zaidi rhumba hilo lilisakatwa wapi na ilikuwa lini. Wote hawa ni marehemu. (Picha kutoka maktaba yetu).*

---

# Ngeli za Nomino

## Hujambo

Na Dkt. Michael Mashauri

**K**ISWAHILI ni miongoni mwa lugha Kizazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tutaendelea na somo la ngeli ambalo hujumuisha majina ya lugha na vitu vingine mbalimbali visivyo na uhai vinavyoanza viambishi **KI-** au **CH-** katika umoja na **VI-** au **VY-** katika wingi. (This noun class includes names of languages and other inanimate things whose names begin with **KI-** or **CH-** in singular and **VI-** or **VY-** in plural.

**Examples:**

Prefixes		Class	Examples		English translation
Singular	Plural		Singular	Plural	
ki-	vi-	KI- /VI-	kiti	viti	chair/chairs
ki-	vi-		kitabu	vitabu	book/books
ki-	vi-		Kiswahili	-	Swahili language
ch-	vy-		chakula	vyakula	food/foods
ch-	vy-		chumba	wumba	room/rooms
ch-	vy-		chandarua	vyandarua	mosquito net/ mosquito nets

Kuna majina mengine ya viumbe hai ambayo huanza na **KI-** katika umoja na **VI-** katika wingi lakini hayaingii katika ngeli hii ila **M/WA** (There are some names for animate things that begin with **KI-** in singular and **VI-** in plural but do not fall under this noun class. They are in **M/**

**WA).**

**Examples:**

kiongozi – viongozi (leader/leaders)  
kipofu – vipofu (blind/blind)

Other names like chai (tea), chupa (bottle) are in **N/N** noun class.

**4.N/N noun class**

Ngeli hii hujumuisha majina ya vitu mbalimbali visivyo na uhai ambayo hayana viambishi vya umoja na wingi (This nouns class consist of various names of inanimate things whose structures do not have singular or plural prefixes)

**Examples:**

Prefixes		Class	Examples		English translation
Singular	Plural		Singular	Plural	
N-	N-	N/N	nguo	nguo	clothes
N-	N-		ndizi	ndizi	banana/s
N-	N-		saa	Saa	watche/s
N-	N-		meza	meza	table/s
N-	N-		nyumba	nyumba	house/s

Majina ya wanyama hayana umoja na wingi lakini yanajumuishwa katika ngeli ya **M/WA** kwa kuwa ni viumbe hai (Animal names have no singular and plural prefixes but they are included in the **(M/WA)** noun class since animals are animate). Examples: simba (lion/s), twiga (giraffe/s), ndege (bird/s).

**•Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

# NEEC ionekane sasa kusaidia Watanzania

Na Tryruckia MFINANGA

**K**ATIKA mizania yoyote ile, maisha ya Watanzania yanaendelea kuwa magumu kila uchao; wanaoishi vijijini wanalia kama wanavyofanya wa maeneo ya mjini.

Wote wanalalamikia mkwamo wa maisha bora kutokana na sababu mbalimbali, zile za asili – kama kukosekana kwa mvua ya uhakika hivyo kukosekana kwa mazao ya chakula na hata biashara na wengine wakieleza serikali kushindwa kusimamia vyema na kurahisisha mifumo ya kutengeneza fedha kwa wananchi wake.

Kwamba badala ya serikali kubuni njia rahisi na zenye kuchochea wananchi kufanya biashara, yenyewe imekuwa ikikandamiza juhudi hizo kwa kuweka kodi kubwa na tozo-umiza lukuki.

Wengi wanajiuliza, hivi hakuna taasisi ama idara yenye kuishauri serikali juu ya namna bora ya kushughulika na biashara za Watanzania; kwamba ishauri kuwekwa kwa uwanja wenye kupanua wigo wa kodi na siyo ongezeko la tozo-umiza nyingi ambazo kimsingi, huzuia ukuaji wa mitaji.

Hivi kazi ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ni zipi kama siyo kuchochea na kushauri serikali iachane na mlolongo wa kodi kwa wafanyabiashara Watanzania?

Katika wavuti ya NEEC, inaonyesha kuwa moja ya majukumu yake ni kuandaa mpango mkakati wa sekta na kisekta na kuhamasisha matumizi ya rasilimali kwa shughuli za uwezeshaji wa wananchi, lakini mpango huo uko wapi, mwananchi anafahamu, au umefungiwa kabatini tu?

Pia inaonyesha kwamba baraza hilo lina kazi ya kuendeleza na kuwezesha shughuli za kibiashara zilizoanzishwa na kuendeshwa na Watanzania, lakini siji wananchi gani wanaozungumzwa hapa. Wengi wahafahamu hata uwepo wa NEEC.



*Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa*

Hivi katika mazingira ya sasa ya maisha ya watu kuwa magumu na upromoka kwa kipato cha mtu mmoja mmoja na hata kaya na taifa, bado NEEC wamelala? Kwanini wapo?

Ni muda muafaka sasa baraza hilo lilaibka na kuja na mikakati inayoonekana wanayo – kusaidia waananchi na kueleza ni ni kifanyike au inafanya nini kuishauri serikali kuhusu malalamiko haya ya ugumu wa maisha unaochangiwa na mifumo ya serikali yenyewe.

Wakati ni sasa wa NEEC kuonekana kuwepo kusaidia wananchi, badala ya kuonekana tu wakati wa mikutano na wakubwa ama wakati wa mafunzo machache kwa wanaotajwa kuwa ni wadau au makabidhiano ya ripoti kadha wa kadha.



## Je, waajiri huiba muda binafsi wa wafanyakazi?



### Na Pericles KALIMANGONGA

**B**ILA kujali kama umeajiriwa serikalini au kwenye sekta binafsi, jukumu la kujinufaisha na mpaka wa kikatiba na kisheria uliopo kati ya muda wa kazi na muda wa maisha ya faragha katika ngazi ya familia, linakuhusu.

Katiba ya Tanzania (1977), chini ya kifungu cha 16(1), inalinda faragha inayoendana na maisha binafsi ya kila mtu awapo nyumbani dhidi ya usumbufu wa mtu yeyote, akiwamo mwajiri.

Kwa mujibu wa Katiba hii, nje ya saa za kazi, marafiki, wanafamilia na wanandoa, wanayo haki ya kuamua wale nini, wanywe nini, walale wapi, walale vipi, waabudu vipi, au wavae nini, bila hofu kutoka kwa mtu yeyote.

Kwenye sekta ya ajira, ulinzi kama huu unapatikana kupitia kwenye sheria kadhaa ikiwamo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (2004) na kanuni zake, pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma (2002) na kanuni zake.

Kwa mfano, ibara ya 19 ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (2004), inakataza mwajiriwa kufanya kazi katika saa za kawaida kwa zaidi ya saa 45 kwa

wiki. Pia sheria inakataza mwajiriwa kufanya kazi katika saa za ziada kwa zaidi ya saa 50 kwa wiki.

Kwa kuwa wiki ina saa 168, kazi zinazofanyika kwenye saa za kawaida kwa wiki hazipaswi kuzidi asilimia 27 ya saa za wiki; na kazi zinazofanyika kwenye saa za ziada hazipaswi kuwa zaidi ya asilimia 30 ya saa za wiki.

Mbali na muda wa kazi, sura nyingine ya sera ya kitaifa kuhusu mpaka stahiki kati ya muda wa kazi na muda wa maisha binafsi, ni likizo ya siku 28 kwa mwaka, likizo ya ugonjwa, likizo ya uzazi,

Kwa hiyo, sera ya kitaifa kuhusu mpaka stahiki kati ya muda wa kazi na muda wa maisha binafsi inaongozwa na kanuni kuu mbili; kuna kanuni ya muda wa kazi na kanuni ya muda wa likizo ya mfanyakazi.

Kama hivi ndivyo, hapa Tanzania, je, waajiri wanaheshimu ukuta wa kisheria kati ya muda wa kazi na muda wa nyumbani?

Mwajiri anayevunja sheria zilizotajwa hapa kuhusu muda wa kufanya kazi na saa binafsi, anapaswa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria.

**Tafakari.**

### ‘Udugu, usawa, utu na Utanzania’

Na Deusedith KAHANGWA

**W**AASISI wa Taifa la Tanzania walitufundisha kuamini kwamba “binadamu wote ni ndugu,” kwamba binadamu wote ni sawa na kila mtu anastahili kuthaminiwa utu wake.

Mawazo haya hayakuanzia Tanzania. Yanao umri wa miaka ipatayo 3000 hivi. Na yalifikia kilele cha ubora wake kupitia udadavuzi wa Immanuel Kant (1724-1804BK) wa Ujerumani aliyefariki akiwa na miaka 79.

Aliandika vitabu kama vile Tahakiki ya Misingi ya Urazini (1781), Misingi ya Metafizikia ya Maadili (1785), Tahakiki ya Misingi ya Maadili (1788) na Tahakiki ya Misingi ya Hukumu (1790).

Kant alifundisha mambo mengi kupitia maandiko yake, lakini atakumbukwa zaidi kwa sababu ya fundisho lake kuhusu umuhimu wa “kanuni ya kuheshimu na kuthamini utu,” yaani “the categorical imperative,” kwa Kiingereza.

Kanuni ya kuheshimu na kuthamini utu, kwa mujibu wa Kant, inasema kuwa; endapo unataka kumtumia binadamu yeyote kama nyenzo ya kufanikisha malengo yako, mara zote zingatia mambo mawili.

Kwanza, epuka kumchukulia kama chombo cha kufanikisha malengo yako pekee, bila kuzingatia ukweli kwamba, yeye pia ni mtu mwenye hazina ya akili timamu na utashi huru.

Na pili, izingatiwe ukweli kwamba, kila binadamu anatomia akili na utashi kuteua mbinu za kufanikisha malengo aliyojiwekea; yakiwemo yale yanayoweza kufanikishwa kupitia ushirika.

Kwa ufupi, mawazo ya Kant kuhusu dhana za “utu” na “ubinadamu” ni zao la uchambuzi na usanisi wa fikra za wanazuo waliomtangulia, wakiwemo Aristoto wa Ugiriki, Anicius Boethius wa Italia, Alan wa Lile huko Ufaransa, Thomas Aquinas wa Italia na John Locke wa Uingereza.



Immanuel Kant

Katika ulimwengu wa falsafa, wanazuoni hawa walitofautisha kati ya “mtu” na “binadamu.” Yaani “persons” dhidi ya “humans”.

Kwa upande mmoja, walifundisha kuwa neno “binadamu” linamaanisha kitu chochote chenye mwili ambao ni kitovu cha hazina ya sifa za hisia, kumbukumbu, urazini na utashi huru.

Na kwa upande mwingine, wanazuoni hawa walifundisha kuwa neno “mtu” linamaanisha kitovu chochote kisicho na mwili chenye kumiliki hazina ya sifa za hisia, kumbukumbu, urazini na utashi huru.

Ni katika mazingira haya, Kant alifundisha kuwa, katika mizania ya utu, kila binadamu bila kujali umri, dini, rangi, jinsi, utafifa, uraia, urefu, unene au umbo, anayo hazina ya urazini na utashi huru.

Akaongeza kwamba, kwa sababu hii pekee, kila binadamu anastahili heshima pamoja na haki sawa na wenzake tangu mimba yake ilipotungwa tumboni mwa mama yake hadi anapoiingia kaburini.

Mawazo ya Kant, hakika yanashabihiana kabisa na misingi ya Utanzania.

**Tumuenzi.**

---

## **Refa akoroga, uwezo wa Mwakinyo waongezeka**

**Na Mwandishi Wetu**

**J**UZI Jumamosi – Septemba 3, 2022 wapenzi wa masumbwi katika sehemu kubwa ya dunia, waliacha shughuli na hata usingizi wao kutazama pambano la Mtanzania Hassan Mwakinyo na Mwingereza, Liam Smith, lililofanyika Liverpool, Uingereza.

Pambano hilo la raundi 12 la uzito wa juu wa kati ( super-middleweight) lililotazamwa na watu wanaokadiriwa kufikia milioni 300 duniani kote, lilianza kwa mabondia wote kusomana, wakirushiana ngumi nyepesi na kujihami zaidi.

Kila bondia alikuwa makini na katika raundi ya pili, Mwakinyo alionekana makini kuliko mpinzani wake, baada ya kumshambulia kwa ngumi mbili za kushtukiza, zilizoanza kumchanganya Smith ambaye alikuwa na mashabiki wengi zaidi kwa kuwa alikuwa akichezea “nyumbani.”

Pambano hilo lililowalazimu mashabiki walioingia ukumbini kulipa kati ya Sh. 142,000 na 851,000, liliingia raundi ya pili, huku Mwakinyo akionekana makini, ingawa alikuwa akiegemea kamba, tofauti na raundi ya awali, ingawa aliendelea kumdhibiti mpinzani wake.

Raundi ya tatu, pia Mwakinyo aliitawala kwa kumdhibiti Smith, huku akimsukumia ngumi za kushtukiza, ingawa nyingi mpinzani wake alizikwepa.

Hata hivyo, mwamuzi alilazimika kusimamisha pambano hilo na kumtangaza Smith kuwa mshindi kwa Technical Knock Out (TKO). Uamuzi huu ulizua tafrani kutoka manajimenti ya Mwakinyo iliyoeleza kutoridhishwa.

Baada ya pambano kumalizwa, Smith alieleza masikitiko yake kwamba ushindi huo hakuutarajia, maana umeisha katika mazingira ya kutatanisha. Hakuelewa nini kimetokea.

Wachambuzi wa mchezo huo kutoka



*Hassan Mwakinyo*

maeneo mbalimbali walisikika wakieleza kwamba ndapo mchezo ungesimamishwa roundi ya tatu – kwa namna yoyote ile, Mwakinyo anetagazwa mshindi, kwani alikuwa amempia Smith ngumi nyingi katika maeneo yenye kukusanya pointi, hasa ya kichwa.

Naye Mwakinyo aliwashukuru Watanzania na mashabiki wake wengine kwa “kumsapoti” na kusema kwamba viatu alivyopewa vilikuwa vinaendelea kumfinya kila muda unaposogea na kumsambabishia misuli ya mguu kukaza, hivyo alilazimika kupiga goti na kutema kikinga mdomo ili kumuonyesha mwamuzi kuwa alikuwa na tatizo.

Hata hivyo, mwamuzi hakujali, bali aliruhusu Smith kuendelea kumshambulia mpinzani wake, hali ambayo ni kinyume na sheria zinazotawala mchezo huo.

Tayari Mwakinyo ameomba kurudiana na Smith wakati wowote.

# PICHA KUBWA



*Serikali imekuwa ikihimiza ulaji wa nyama; iwe ya mbuzi, kondoo, ng'ombe au hata jamii ya ndege ikiwa ni pamoja na kuku, bata, kanga, njiwa na wengine. Hapa ni eneo la kuchoma nyama ya mbuzi kama lililovyokutwa juzi na mpigapicha wetu katika Mnada wa Namdende, mjini Handeni, Tanga.*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

